HOTUBA YA JAJI MKUU MOHAMED CHANDE OTHMAN

KATIKA SIKU YA SHERIA NCHINI

TAREHE 2 FEBRUARI 2011

Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Anna Makinda, Mb., Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Celina Kombani,Mb. Waziri wa Katiba na Sheria;

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani;

Mhe. Jaji Kiongozi;

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu;

Wahe. Majaji Wakuu Wastaafu na Majaji Wastaafu;

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mhe. Msajili wa Mahakama ya Rufani;

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanzania Bara;

Wh. Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;

Wasajili; Mahakimu; Mawakili

Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Viongozi wa dini;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.

<u>Mheshimiwa Rais,</u> Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uhai na afya njema, na kutupa uwezo wa kukusanyika hapa hii leo. Namshukuru pia kwa uchanguzi mkuu wa amani na utulivu uliofanyika mwishoni mwa Oktoba mwaka jana, 2010.

Aidha, nachukua nafasi hii kukupongeza Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kingine cha miaka mitano [2010 – 2015]. Naamini sijachelewa sana kutoa pongezi hizi.

Pili, napenda kukukaribisha Mhe. Rais, Mhe. Spika, Mh. Waziri wa Sheria na Katiba na Waheshimiwa wageni wote mliohudhuria kwenye sherehe yetu ya siku ya sheria inayoashiria mwanzo rasmi wa mwaka wa kimahakama, kote nchini.

Mhe. Rais, kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania na kwa niaba yangu mwenyewe, natoa shukrani za dhati kwako kwa kukubali kwa mara ya nne mfululizo tangu mwaka 2008, kuwa tena nasi kwenye sherehe yetu punde tuu baada ya safari ndefu.

Mh Rais, umetuzoesha kuchova asali; tuwiye radhi kuichovya!.

Namshukuru pia Mh Speka kwa kuwa nasi. Najua una majukumu mengi ya kutayarisha kikao kijacho cha Bunge letu tukufu kinachoanza Dodoma tarehe 8 Februari 2011.

Mhe. Rais, maudhui ya siku ya sheria mwaka huu ni:

> **"UMUHIMU wa ELIMU kuhusu Mahakama kama hatua ya msingi ya utatuzi wa migogoro katika jamii."**

Mhe. Rais, Katika Dira ya taifa ya maendeleo ya mwaka elfu mbili na ishirini na tano (2025), moja ya lengo linalotarajiwa ifikapo mwaka huo ni:

“Tanzania kuwa na jamii ILIYOELIMIKA na inayopenda KUJIFUNZA zaidi.”

<u>Elimu kuhusu mahakama</u>

Elimu ya ukweli, alivyo tufundisha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ni lazma iwe na madhumuni haya:

“The liberation of Man from the restraints and limitations of ignorance and dependence”.

Tafsiri: ‘Kumkomboa Mtu kutoka kwenye KIZUIZI na KIZUIO cha ujinga na tegemezi’.

Mh Rais, tukizingatia hilo, elimu kuhusu Mahakama ni lazima ilenge kumkomboa mwananchi kutoka kwenye athari

anazozipata kwa kutoielewa vyema Mahakama na sheria. Elimu au uelewa tunaouzugumzia hapa ni ule wa msingi. Sio wa shahada ya sheria.

Mh Rais, kama unavyofahamu mara nyingi migogoro huletwa Mahakamani ikiwa kimbimlio la mwisho la mwananchi baada ya usuluhishi kwenye jamii kushindikana. Kwenye usuluhishi, wanaopatanishwa wote huwa washindi. Kinyume, Mahakamani kuna mshindi na mshindwa. Wananchi wengi, haswa wale wenye kipato kidogo hujiwakilisha wenyewe. Na sio wasomi. Kwa hiyo, uelewa wa Mahakama utawasaidia sana kujiandaa kikamilifu wanapopeleka dai au anapotakiwa kujibu dai. Wataelewa vizuri uamuuzi, sababu zake na tuzo itakayotolewa.

Mh Rais, Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inasema hivi:

Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji HAKI katika Jamuhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama.

Mh Rais, Pamoja na hilo, Mahakama pia ina jukumu la kutafsiri sheria. Mara nyingi tafsiri ya sheria inawapa fumbo wasomi. Jee kwa wananchi itakuaje?.

<u>Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu Mahakama na sheria</u>

Mh Rais, ni msingi wa sheria kwamba kila mtu anatarajiwa kujua sheria. Kutokuijua sheria; sio kinga (Ignorance of the law is no excuse). Na kwa bahati mbaya, uelewa wa wananchi kuhusu Mahakama na sheria ni mdogo. Bado ni kitendawili!

Mh Rais, ujinga tunaouzumgumzia hapa unamaanisha KUTOELEWA. Huongeza athari. Hili halihusu haki tuu, bali hata afya na uchumi. Kwa mfano, watu wengi, miongoni mwetu, nadhani tunajua tuu juu ya saratani ya ngozi, ya kizazi , ya matiti na ya kibofu cha mkojo. Zote zinaua.

Kwa heshima kubwa, sidhani kama tunajua kwamba pia kuna saratani ya ulimi inayoua na inayotokana na matumizi ya kupindukia ya unywaji pombe na uvutaji sigara!. Wengi tunadhani saratani haiepukiki!. Ni bahati mbaya!. La hasha,

makali ya saratani yanapunguzika!. Elimu ni nusu dawa.

Mh Rais, hata kwenye uchumi na maendeleo, uelewa mdogo unaleta athari. Mtu asipoelewa, anaweza kuwa na fikra potofu ya kiuchumi kwamba watanzania wote tunaweza kuwa matajiri haraka haraka kwa kuchapisha noti nyingi na kuzigawa!. Kutoelewa uchumi hata chembe kunaweza kumfanya mwananchi apuze bidii ya kujiendeleza.

Mh Rais, mwaka elfu mbili na tisa (2009) asilimia ishirini na saba nukta saba (27.7 %) ya Watanzania waliokua na umri

zaidi ya miaka 15 walikua hawajui kusoma wala kuandika lugha yoyote (Human Development Report, 2009).

Pamoja na lengo jema la Serekali kufuta hilo ifikapo mwaka elfu mbili na kumi na tano (2015), havi sasa tuna wenzetu ambao hawakujaaliwa. Tusitegemee wananchi hawa kujua sheria na kanuni za Mahakama ambazo saa nyingine hutatanisha.

Muelewa hababaishwi wala hababaiki. Elimu juu ya Mahakama itamuezesha mwananchi kutetea haki zake kikamilifu, ndai na hata nje ya Mahakama.

<u>Kusambaza Elimu kuhusu Mahakama: Jukumu la pamoja</u>

Mh Rais, kwa upande wetu, Mahakama imefanya mambo kadhaa kuelimisha wananchi. Kila mwaka tunashiriki kikamilifu katika maonyesho ya sabasaba ambako Wananchi hupata fursa ya kuelimishwa. Mahakama imetoa vipeperushi mbalimbali vinavyoelezea shughuli zake. Kubwa zaidi, tumechapisha kijarida cha mkataba wa huduma kwa mteja

(Client Service Charter). Kijarida hiki kimeelezea shughuli za Mahakama, viwango vya huduma, haki za wateja na namna ya kutoa malalamiko. Pia, tulizindua tovuti ya Mahakama Decemba 2010.

Mh Rais, jitihada za Mahakama pekee hazitoshi. Nachukua fursa hii kukaribisha mchango wa Chama Cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Vyama Vya Msaada wa Sheria (Legal Aid Organziations), Asasi za Haki za Binadamu na Vyombo vya Habari ili tusaidiane kukamilisha jukumu hili la kuwaelimisha wananchi. Umoja ni nguvu!

<u>Uwezo wa Mahakama kutoa haki sawa na kwa wakati</u>

Mh Rasi, kuna uwiyano mkubwa kati ya uwezo wa Mahakama kutenda haki na umalizikanaji wa kesi. Kama unavyojua, Dira ya Mahakama ni kutoa haki kwa wote na kwa wakati. Mwelekeo wetu, ni kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi

kwenye mazingira ya haki, uwazi na yanayozingatia maadili ya utendaji kazi.

<u>Utoaji haki na Mfuko wa Mahakama</u>

Mh Rais, kwa upande mwengine, elimu kuhusu Mahakama inaweza kuzua mzigo. Shauku ya wananchi kudai haki zao, ambayo tunaikaribisha, itaongeza idadi ya migogoro Mahakamani. Na sio siri, kwa sasa mlundikano HAUJATOKOMEA. Hili, kama mbala mwezi halifichiki! Jee linaelezeka? Linatibika?

Mh Rais, kwa mwaka 2008/2009 kati ya kesi 61,237 zilizokua Mahakama za Hakimu Mkazi wa Mkoa na wa Wilaya, kesi 42,725 zilihitimishwa. Kwa mwaka 2009/2010 kati ya kesi 62,154 kwenye Mahakama hizo, kesi 46, 997 zilimalizika. Kiwango cha kumaliza kesi kwa miaka hiyo kilikua asilimia sitini na tisa nukta nane (69.8 %) (2008/2009) na asilimia sabini na tano nukta sita (75.6 %) (2009/2010).

Mh Rais, kwenye Mahakama za Mwanzo, kwa mwaka 2008/2009 kati ya kesi 213, 239 zilizokuepo, kesi 151, 200 zilimalizika. Na kwa mwaka 2009/2010 kati ya kesi 218, 767 kesi 167,228 zilifikia kikomo. Yaani, asilimia sabini nukta tisa (70.9 %) (2008/2009) na asilimia sabini na sita nukta nne (76.4 %) (2009/2010) ya kesi ndio zilizohitimishwa. Ni Wazi, tuna kiporo! Kwa hili, kama wasemavyo wahenga: kosa moja haliachi mke wala mume!.

Mh Rais, pamoja na hali hii isiyoridhisha, picha kamili ni kwamba Mahakama za Hakimu Mkazi wa Mkoa na wa Wilaya zilimaliza kesi 4,272 zaidi mwaka 2009/2010 kuliko mwaka 2008/2009. Na Mahakama za Mwanzo hivyo hivyo zilifanya bidii INAYOONEKANA kwa kumaliza kesi 16,028 zaidi mwaka 2009/2010 kuliko mwaka 2008/2009. Juhudi zinafanyika. Tutajituma zaidi.

Mh Rais, Mahakama itaendelea na mikakati maalum ya kuongeza kasi ya usikilizaji na umalizikaji wa kesi. Tutakumbushana. Tutawajibishana. Tutarekebisha kanuni zenye mafumbo. Tutarahisisha taratibu. Tutabadilisha zile la kale. Tutawaelimisha zaidi na kuwasimamia Mahakimu. Tutawaandika Majaji Wastaafu. Na kama ilivyotuelekeza Ibara 107 (2) (e) ya Katiba tutatia maanani utendaji haki bila kufungwa sana na masharti ya kiufundi.

Pamoja na hayo, Mh Rais, tutashirikiana na wahisani wetu wanaochangia kwenye Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (Legal Sector Reform Programme) na MKUMBIA (Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST-Better Business Environment Strengthening for Tanzania) zikiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, Denmark, Sweden, Uholanzi na Uingereza. Pia tutaongeza uhusiano na Investment Climate Facility for Africa (ICF). Ushirikiano huu, utatuwezesha kutumia zaidi mifumo ya teknologia ya

uendeshaji wa mashauri na ule wa kuhifadhi kumbukumbu. Yote haya yatachangia sana kuwapunguzia Watanzania adha Mahakamani. Mageuzi haya, Mh Rais, yako mikononi mwetu. Yataharakisha utoaji haki.

Mh Rais, kama unavyofahamu, hilo ni jibu la upande moja. Wasemavyo wahenga: mkono moja haulei mwana!

Mh Rais, nchi yetu ina stahili kujivuna. Hatuna tatizo la kuingiliwa kwenye Uhuru wa Mahakama.

Changamoto kubwa zinazoikabili Mahakama na ZINAZOCHANGIA kwa sehemu kubwa, ulimbikizaji wa kesi Mahakamani ni kwamba bajeti yetu, finyu, hailingani kabisa na haizingatii mahitaji halisi ya Mahakama.

Mhe. Rais, katika mwaka wa fedha 2008/2009 mahitaji yetu na fedha tulizoomba zilikuwa Tsh 93 bilioni, lakini

tulitengewa Tsh 50.2 bilioni, ambayo ilikuwa ni asilimia hamsini na nne (54%). Kati ya hizo, hatimae tulipata Tz shs 44.4 bilioni, ambazo pia zilikua pungufu kwa asilimia kumi na mbili (12 %). Hali hiyo inaedelea.

Mh Rais, mipaka ya bajeti (budget ceiling) tuliyowekewa haizingatii kabisa hatua iliyopiga Mahakama. Tangu 2005, Mahakama Mkuu imeogezeka kwa kanda 2 za Iringa na Sumbawanga. Tumefungua Mahakama za Wilaya 11 kwenye Mikoa 9.

Mh Rais, pia fedha zilizoidhinishwa na Bunge tukufu hazitumwi kamili; haziletwi kwa wakati, na huletwa punje punje. Kwa mfano fedha zilizotengwa kwenye mgao wa bajeti wa mwezi Augosti 2010 kwa ajili ya Mahakama zilikua pungufu kwa asilimia tisini na saba (97 %) kulinganisha na bajeti iliyokubaliwa. Kufikia Decemba 2010, kwenye mafungu

husika, tulipokea fedha ambazo zilikua asilimia thelathini (30%) pungufu kuliko zile zilizoainishwa.

Mh Rais, matokeao ya haya ni kwamba badala ya vikao 6 vya kusikiliza mashauri mbali mbali ya mauaji katika kanda 13, Mahakamau Kuu iliweza kufanya vitako 3 tuu; na badala ya vikao 15 vilivyopangwa, Mahakama ya Rufani, iliweza kufanya vikao 10 tuu. Tulishindwa kuita mashahidi. Wazee wa Baraza, hua hawalipwi. Na wanatudai Tz shs 61 milioni.

Mh Rais, changamoto kubwa nyingine ni upungufu mkubwa wa Mahakimu na Majaji; ukosefu na uhaba wa miundo mbinu na vitendea kazi na ucheleweshwaji wa mafao na stahili. Kama kutatokea mlipuko wa utoaji haki, basi mchanganyiko huo ndio chimbuko. Kwa heshima, Mh Rais, tiba ya serekali ndio dawa.

Mh Rais, Mahakama ilifarijika sana tarehe 18 Nov. 2010 wakati unazindua rasmi Bunge la kumi la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, ulivyoweka mkazo haya kwa jina la Serekali:

"*Tutaendelea kuongeza bajeti ya Mahakama nchini. Tutakamilisha mchakato wa kuanzisha mfuko wa Mahakama ambao utaongeza uhuru na uwezo kwa masuala ya fedha na rasilimali*".

Mh Rais, tunatanguliza shukurani zetu za dhati kwa ukamilishaji wa mpango huo. Utaipa Mahakama mfuko wake kama ilivyo kwa muhimili mwingine, Bunge letu tukufu.

Mh Rais, kama usiku unavyofuata mchana, baada ya mfuko kuzaliwa litajitokeza swala la kiwango cha kuweka ili mfuko ufanye kazi. Kwa heshima kubwa niwiye radhi kwa kuleta ombi juu ya ombi! Ili kukidhi kikamilifu mahitaji halisi ya

utaoji haki na Mahakama NAKUSIHI kama alivyonitangulia Mh. Jaji Mkuu mstahafa, Augustino Ramadhani, Serekali ifikirie kutoa asilimia mbili (2%) ya bajeti ya mwaka kama kianzio kwenye mfuko wa Mahakama.

Mh Rais, kitaifa tukifanikiwa hayo hakuna shaka yoyote kuwa serekali ya awamu ya nne unayoiongoza itawacha kama ritisha (legacy) Muhimili unaojitosheleza kiutendaji haki na sio Muhimili TEGEMEZI. Nchi yetu itakua na sababu ya pili, nzito, ya kujigamba.

Mh. Rais wewe ndiyo kimbilio letu. Tunaamini kilio chetu utatufuta machozi, kama ulivyofanya mara kadhaa hapo nyuma.

<u>Utoaji haki na Mahakama za Mwanzo</u>

Mh Rais, niwie radhi, niziongelee kidogo Mahakama za Mwanzo. Nizipigie mbiu!. Maudhui ya mwaka huu yatakua pungufu, nikizipuuza.

***Kwanza*, Mahakama za Mwanzo ambazo ndio ngazi ya chini ya Mamlaka yetu ya utoaji haki ni tegemeo la wananchi wengi, haswa vijijini. Kisheria ni Mahakama za Mwanzo. Ki utendaji haki ni Mahakama za jamii. Mwaka 2009/2010 tuu ,Mahakama za Mwanzo zilikua na kesi 218,767. Kwa idadi hii, takriban katika kila watanzania mia moja na themanini na saba (187) – mmoja alikua na kesi Mahakama ya Mwanzo.**

***Mh Rais,* pili, hivi sasa kuna vituo vya Mahakama za Mwanzo 974 vinavyofanya kazi. Ili haki sawa itendeke kwa wote na nchi nzima mahitaji yetu ni vituo vya Mahakama za Mwanzo 1105. Tuna upungufu wa vituo 131.**

Kuna sehemu nchini hazina kabisa Mahakama. Wananchi hufunga safari ndefu kutafuta haki zao, na kwa gharama. Mwanya huu, huwabagua. Hawatendewi haki.

Mh Rais, *tatu*, Mahakama ina Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 760. Vituo vyetu vya Mahakama za Mwanzo ni 974. Kuna uhaba mkubwa wa Mahakimu. Na hakuna ajira ya Mahakimu iliyoidhinishwa mwaka huu wa fedha, mpaka sasa.

Mh Rais, hivi sasa Mahakimu huhudumia Mahakama za Mwanzo zilizopo mbali sana na makazi yao. Tuna Mahakama za Mwanzo 551 zinazopata huduma kwa kutembelewa na Mahakimu. Ki uoaji haki, ni Mahakama za Mwanzo za msimu!

Kwa mfano, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya MPANDA, Sumbawanga anahudumia Mahakama ya Mwanzo ya MISHAMO ambayo iko umbali wa kilometa 130. Yule wa Mahakama ya Mwanzo ya MTOSIWA anatembelea Mahakama ya Mwanzo ya KIPETA, karibu kilometa 117.

Huko, Mtwara, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya MSIMBATI anahudumia Mahakama ya Mwanzo ya

NANYAMBA, ambayo iko kilometa 113. Mkoa wa Lindi, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo wa MITEJA (Kilwa) anahudumia Mahakama za Mwanzo za KIPATIMU na CHUMO. MITEGA mpaka KIPATIMU ni kilomita 70 na KIPATIMU kwenda CHUMO ni kilomita 110.

Mara nyingi tunashindwa kuwalipa Mahakimu hawa posho. Wengi hujilipia nauli. Walio bahatika kuwa na Pikipiki ya Mahakama, huweka mafuta kwa fedha zao wenyewe. Saa nyingine,Mahakimu hawa wanajiuliza: Jee haya ni mazingira magumu au mateso?

Mh Rais, kwenye sera na mikakati ya elimu, Serekali imeleta matumaini ya kishindo. Hakuna Mkuu wa Shule ambae anasimamia kwa wakati moja, shule mbili ambazo ziko umbali

wa kilomita 130 baina yao. Kwa mantiki hiyo, hili la Mahakama na Mahakimu linatibika.

Mh Rais*, tano, MAJENGO* mengi ya Mahakama za Mwanzo hayana staha. Mahakama ya Mwanzo ya Kate (Sumbawanga) iko kwenye jengo lililokua ghala ya kijiji. Zile za Katoro (Geita) na Mugeta (Bunda) ziko kwenye ghala ya mazoa.

Huko Mtwara, ile ya Chikundi iko katika jengo la soko la kijiji na ya Nachingwea iko kwenye jengo lililokua klabu ya pombe. Zile za Kilimarondo na Ndomoni (Lindi) ziko kwenye gulio.

Mh Rais, *sita,* Mahakama inamiliki majengo ya Mahakama za Mwanzo 614 tuu kati ya 974. Majengo ni machakazu au mbavu za mbwa! Pamoja na nia njema ya Serekali TUNAYOITHAMINI SANA, kinacho leta majonzi, Mh Rais ni kwamba fedha za maendeleo ilizopewa Mahakama kwenye

bajeti ya mwaka 2010/2011 ni za kujenga Mahakama za Mwanzo MPYA tano (5) tuu nchi nzima.

Tunashukuru sana wafadhili waliochangia kwenye Programu ya Marekebisho ya Sekta ya Sheria (LSRP) utakaotuwezesha kujenga Mahakama za Mwanzo 20 mpya mwaka huu.

Mh Rais, pia nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi ambao mara nyingi huchangia nguvu kazi kweye ujenzi wa mahakama hizi kama zile za Nandembo, Tunduru; Sopa, Sumbawanga; Kiomboi, Iramba; Dongobesh, Mbulu na Kanyana, Serengeti. Wananchi, bado wana imani na Mahakama hizi.

Mh Rais, kwa fadhila zako na kwa heshima kubwa naiomba serekali iwe na upendo zaidi na Mahakama za Mwanzo! Naazima msemo wako Mh Rais, iwe na Upendo kama wa Mama!

Wakati umefika wakuziweka Mahakama za Mwanzo kwenye kilele cha utawala bora, utawala wa sheria na utoaji haki.

Mh Rais, tutashrikiana kikamilifu na Mh Waziri Mkuu na Ofisi yake, Wizara ya Sheria na Katiba, Mamlaka za Mikoa na za Wilaya pamoja na Halmashauri ili tuweze KUJENGA, KUENDELEZA NA KUUIMARISHA Mahakama hizi. Jitihada maalum zinahitajika. Bila ya hilo, juhudi zetu za kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini zitakuwa hadithi.

<u>Utendaji haki na raslimali watu</u>

Mh Rais, tangu uingie madarakani mwaka 2005 umeteua majaji 52 wa Mahakama Kuu na Majaji 12 wa Mahakama ya Rufani. Haijawahi kutokea tangu tupate uhuru miaka 50 iliyopita. Unastahili kupongezwa kwa shangwe na vifijo (vigelegele). Pamoja na upendeleo huu, Mh Rais, bado tuna

kiu. Kasi ya wastaafu imemega idadai hii ya Majaji. Hivi sasa tuna Majaji 62 kwenye kanda 13 za Mahakama Kuu.

Mh Rais, Tanzania tuna Majaji 2 tuu kwa kila watu 1,064,000. Mwaka 1987, zaidi ya miaka 23 iliyopita, kwa kila watu milioni moja India ilikua na Majaji 10, Australia 41, Uingereza 50, Canada 75 na Marekani 107. Hatuthubutu kuiga. Kwetu uwiano wa Majaji na Mahakimu na idadi ya watu, haviendani. Hailingani na wingi na uzito wa kesi Mahakamani wala matakwa ya utendaji haki kwa wakati. Kwa mfano, mbele ya majaji 5 wa Mahakama Kuu, Divisheni ya Ardhi hivi sasa kuna kesi 2008, na mwaka huu tunategemea nyingine zaidi ya 1000 kuletwa. Kila moja yao atakua na kesi zaidi ya 600 mwaka huu tuu.

<u>Hitimisho</u>

Mh Rais, kwa kumalizia, maudhui ya mwaka huu yametia maanani elimu juu ya Mahakama kama msingi wa utatuaji wa

migogoro kwenye jamii. Hii inaenda sambamba na Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka elfu mbili na ishirinni na tano (2025) inayolenga nchi yetu kuwa na jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi.

Mh Rais, busara inasema:

“There is no wealth like knowledge; no poverty like ignorance.”

Yaani: Hamna UTAJIRI kama elimu; hamna UMASKINI kama ujinja (uelewa).

Nakushukuru sana Mh Rais, kwa hisani uliyotutendea kuwa nasi hii leo. Kuadhimisha Siku ya Sheria namna hii kunathibitisha umoja na ushirikiano mkubwa kati ya Mihimili mitatu ya serekali yetu. Kuja kwako Mh Rais, na Mh Speka kunaipa NEEMA siku hii muhimu ya Mahakama, nchi nzima.

Mh Rais. Sio nia yangu kuleta ombi. Nimekuletea yakutosha. Wewe mwenye umahiri wa kuwasoma Wananachi zaidi kuliko mimi, nadhani umeshatambua kuwa wana shauku kubwa kusikia sauti yako, hata kama ni kuwasabahi tuu.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Nawatakia kheri na baraka za mwaka mpya wa Kimahakama.